


Hii gazeti ina andikwa na shirika lisilokuwa la kiserekali Internews kwa ushirikiano na wizara ya afia na Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekunda na Jumuiya Nyekunda kwa kujibu kwenyi mahitaji za habari ya jamii.

Kila juma, tunakusanya na kuchambuwa maioni ya jamii (uvumi yani habari zenyi hazina uhakika, wasiwasi, maulizo, na kazalika) na tunatafuta majibu ku toka kwa wataalamu kwa kushirikisha jamii. Maulizo hizo zinachunguzwa kulingana na maana(umuhimu) yazo na mwendeleo wazo.

Fuateni habari za jibu juu ya Ebola katika gazeti ya Radio "Koma Ebola"

soundcloud.com/user-740750674
Facebook.com/komaebola
[@Ebolakoma](https://Twitter.com/@Ebolakoma)
koma-ebola.info



EBOLA

SWALI

Juu ya nini janga (ma épidémies) zote zina ambukia kupitia mikono?

JIBU

Janga zote hazina msinji moyo na haziambukie namna moyo. Zimoya zinaweza tokana na tabia, na mazingira ya batu na zingine zinaweza tokana na uchafu (microbes). Mara mingi ni zile zenyi zinatokana na microbes njo zinaambukia kupitia mkono. Uzowefu (experience) inaonyesha kama tunatumia mikono yetu zaidi ya mara miya saba kwa siku, njo maana mkono ni moyo ya njia za kawaida za kuambukizia magonjwa mingi.

CORONAVIRUS

SWALI

Namna gani mutu mwenye iko suspect wa virus ya corona atajuwa kama amekamatika bila kuonyesha alama (signes)?

JIBU

Kila mutu anaweza kuwa suspect wakati anaonyesha ma signes. Juu ya COVID-19, batu ba mingi benyi bana shikwa nayo habiko banaonyesha ma signes za kuonekana sawa vile homa na mchoko. Njo maana inawezekana kuambukizwa na COVID-19 na mutu mwenyi hana hata signe moyo lakini ma analyses ku laboratoire tu njo zinaweza hakikisha (confirmer) kama mutu iko na virus.

Na njo maana inashauriwa kwa kila mutu mwenyi iko suspect kwenda haraka ku kituo cha afia cha karibu kwa kujipimisha ili apate kufaidika na matunzo.



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE




**TRANSLATORS
WITHOUT BORDERS**

**PAUL G. ALLEN
FAMILY FOUNDATION**



Internews
Local voices. Global change.





**TULISIKIA PA
BUTEMBO
KUHUSU EBOLA**
May
(Mwezi wa Tano)
2020

**TULISIKIA PA
BUTEMBO
KUHUSU CORONAVIRUS**
May
(Mwezi wa Tano)
2020

EBOLA

SWALI

Je! kuko ginsi ya ku isoler benye balioponaka Ebola kwa kuepuka maamubukizi juu mulituambiaka kama ni bale benye balioponaka njo baliletaka tena ugonjwa?

JIBU

Mpaka sasa, hakuna mutu wa timu ya riposte mwenyi alihakikisha kama ni benye balioponaka njo banatumaka ugonjwa ya virus ya Ebola inajitokeza tena mu eneo zenyi ziliguwa. Ku isoler benye balioponaka ni sawa namna ya kubashota kidole na kubabagua. Kuko mpango (programme) kamilifu ya kufutilia benye balioponaka Ebola yenyi inabapatiaka msaada ya matunzo na kisaikolojia yakukamilisha kama benye balioponaka habiko hatari ya kujitokeza tena kwa ugonjwa.

Ni ya lazima kuitika kuishi na benye balioponaka Ebola na kubapatia moyo baendeleye kufuata mashauri banayopewa wakati bako banafuata matunzo.

Kwa kuepuka maambukizi, inashauriwa siyotu kwa benye balioponaka lakini na kwa jamii yote kuendelea kuheshimia kanuni za kujikinga.

CORONAVIRUS

SWALI

Juu ya nini munatuomba tukuwe tunasukula mikono na japo COVID-19 inashambulia njo njia za kupumulia?

JIBU

Kusukula mikono saa zote inapunguza maambukizi ya virus ya aina ya virus ya corona na magonjwa zingine za mingi zenyi kuambukia kupitia uchafu. Virus ya Corona inaambukia kupitia njia ya kupumulia kwa ma toni za kidogo kidogo za mate zenyi mgonjwa anatosha (saa yenyi anasema, saa anakohola, na saa anachafia).

Kwa ajili ya makingo, bakubwa benyi kuhusika na afia bana tiya mkazo (insister) batu baheshimie kanuni za afia zenyi zinaomba batu kusukula mikono mzuri na saa zote bakitumia mayi safi na sabuni, kuachiana distance au moins ya metre moyo na batu bengine, na kutumikisha maske muzuri, na kazalika.

Hii gazeti ina andikwa kwa msaada wa watu wa Amerika kupitia Shirika ya Amerika kwa maendeleo ya kimataifa (USAID).

Yaliyomo haionyeshi maoni ya USAID na serikali ya Amerika.



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE

